

## KUTHIBITI KUINGIA MWEZI WA RAMADHAN.

Kuthibiti kuingia mwezi wa Ramadhan ni moja kati ya haya mambo yafuatayo;  
1. Kuonekana kwa mwezi wa Ramadhan, ukionekanwa mwezi basi ni wajibu kufunga.

Mtume (saw) anasema:

(Mtakapouona mwezi fungeni, na mnapouona fungueni) (Amaeipokea Bukhar na Muslim:1900, 1080).

Inatosha kuthibitisha kuonekana kwa mwezi wa Ramadhan mtu mmoja muadilifu, ama kuokana kwa mwezi wa shawwal kwa ajili ya kufungua ni kushuhudia watu wawili waadilifu.

2. Kukamilika kwa mwezi wa Sha'aban siku thelathini, itakapokamilika siku ya thelathini na moja basi hiyo ndio siku ya kwanza ya mwezi wa Ramadhan.

Mtume (saw) anasema:

(Utakapozibwa kwenu na mawingu msiuone, basi kamilisheni hesabu ya siku thelathini za mwezi wa Sha'aban)

## WALIORUHUSIWA KULA MWEZI WA RAMADHAN. (KUFUNGUA).

1. Mgonjwa ambae anatarajiwa kupona ikawa ni tabu kwake kufunga, ye ye anaruhusiwa kufungua, kisha atazilipa zile siku alizofungua siku nyingine, ikiwa mtu ana maradhi endelevu atarajiwi kupona, haimlazimu kufunga, lakini atalisha kila siku masikini mmoja kilo moja na nusu ya mchele au mfano wake au atapika chakula atamuita masikini aje kula kwa idadi ya siku alizofungua.

2. Msafiri: Inafaa msafiri kufungua mwanzo wa safari yake kutoka mji anaishi mpaka ataporudi ikiwa hajatia nia ya kuishi huko alikokwenda.

3. Inafaa kwa mwanamke akiwa na mimba au kunyonyesha atakapo ogopea nafsi yake na mtoto wake atafungua, ukiondoka udhuru atazikidhi zile siku alizofungua.

4. Mtu mzima (Mzee) ambaye ni tabu kufunga, anaruhusiwa kufungua bila ya kuzikidhi siku zilizompita, lakini atalisha kila siku masikini.